



Miaka 10 ya e-GA



Ushirikiano na Zanzibar wachochea kukua kwa serikali ya kidijiti

Na Mwandishi Maalum

Katika kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika, ni jambo la kujivunia kuona pia ushirikiano wa taasisi za umma Tanzania Bara na Zanzibar ukiimarika. Ushirikiano huu ni msingi katika kuleta maendeleo ya taifa letu kwa ujumla.

Hii inadhihirishwa na jinsi ambavyo Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) inashirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) katika jitihada za kukuza Serikali Mtandao kwa pande zote mbili, lengo ni kuhakikisha kuwa jitihada hizo zinatekelezwa kote bara na Visiwani.

Ushirikiano huo umekuwa ni nguzo kwa taasisi hizi mbili tangu kuanzishwa kwake ambapo Mamlaka ya Serikali Mtandao imekuwa ikifanya kazi kwa ukaribu na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzoefu sambamba na kutoa msaada wa kiufundi inapohitajika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar, Bw. Said Seif Said amesema kuwa, Wakala hiyo na Mamlaka ya Serikali Mtandao zimekuwa na mahusiano pamoja na mashirikiano mazuri katika jitihada za kukuza serikali mtandao.

“Taasisi hizi mbili zimeshasaini Mkataba wa Makubaliano (MOU) ili kuimarisha ushirikiano na kuhakikisha Jitihada za Serikali Mtandao zinafikiwa kwa ukamilifu kwa pande zote mbili za muungano bila kuacha nyuma upande mmoja” amesema Seif.

Aidha, Bw. Seif ameongeza kuwa matokeo ya mashirikiano hayo yameweza kuonekana katika utengenezaji na uimarishaji wa mifumo ikiwemo kusaidiana kitaalamu, kushauriana na kupeana mafunzo baina ya wataalamu wa Taasisi hizi mbili ikiwemo matumizi ya mfumo wa Barua Pepe za Serikali, mfumo wa uendeshaji wa Baraza la Wawakilishi, mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroni (Zanmalipo) na Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-office).

“Mwanzoni tulikuwa tunapata tabu katika matumizi ya mfumo wa barua pepe za Serikali lakini kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao tumeweza kuwa na mfumo wa barua pepe za ofisi ambazo zinatumiwa na serikali ya Zanzibar”, amesema Bw. Seif na kuongeza kuwa,

Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao, Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar inatumia mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki ujulikanao kama ‘ZanMalipo’ ambao umeisaidia sana Serikali ya Zanzibar katika ukusanyaji wa mapato kwa Taasisi za Umma. Mfumo huu umesanifiwa na kutengenezwa kwa ushirikiano wa taasisi hizi mbili.



Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar, Bw. Said Seif Said akielezea kuhusu ushirikiano wa e-GA na eGAZ

Kutokana na matokeo mazuri ya ushirikiano huu katika kujenga taifa la kidijitali, Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar imeahidi kuendeleza na kuimarisha ushirikiano huo ambao umedumu kwa muda mrefu pamoja na kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao kutimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake.

“Ushirikiano huu una nia njema ya kuijenga Tanzania ya kidijitali na kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kiutendaji yatakayohakikisha wananchi wanapata huduma bora na rahisi muda wowote na mahali popote”, amesema Seif.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Bi. Mansura Kassim ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa jitihada zake za kukuza Serikali Mtandao na kuhakikisha utoaji wa huduma za serikali kwa njia ya kidigitali unaimarika, na hivyo kuongeza ufanisi katika utendaji kazi serikalini.



“Mamlaka ya Serikali Mtandao imeisaidia Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar kupata uzoefu na ujuzi wa kusanifu na kujenga mifumo mbalimbali iliyosaidia utoaji wa huduma za Serikali kwa ufanisi” amesema Bi. Mansura na kuongeza kuwa,

Miongoni mwa mifumo hiyo ambayo hadi sasa Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar inajivunia ni pamoja na mfumo wa Ajira ujulikanao kama ‘ZanAjira’ unaotumika kutangaza nafasi mbalimbali za kazi kwa wananchi.

“Mfumo huu umesaidia kupunguza malalamiko ya upatikanaji wa ajira na kuleta usawa kwani kila mtu anapata fursa ya kuomba ajira na hivyo kujenga imani kwa wananchi juu ya Serikali yao” amesema na kusesitiza kuwa,

Serikali ya Zanzibar itaendeleza na kuimarisha ushirikiano na Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuhakikisha utoaji wa huduma za Serikali kwa njia mtandao unaendelea kuimarika.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba, amewashukuru viongozi wa Serikali na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar kwa kuendelea kuimarisha mahusiano mazuri ya taasisi hizi mbili.

“Tunafanya kazi kwa ukaribu sana na wenzetu wa Zanzibar, tunabadilishana uzoefu na maarifa pamoja na kutoa msaada pale inapohitajika kwa lengo la kujenga na kuimarisha serikali mtandao Bara na Visiwani” amesema Ndomba.

Aidha, Ndomba ameeleza kuwa, ushirikiano ni moja ya misingi inayoiongoza taasisi hiyo ili kufikia malengo iliyojiwekea na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi mkubwa.

Ndomba ameitaja misingi mikuu sita (6) inayoiongoza Mamlaka hiyo ambayo inaelekeza kuhusu tabia na mwenendo wa watumishi wake kwa ngazi zote sambamba na kufafanua utamaduni wa mahali pa kazi, ili kuhakikisha watumishi na wateja wote wa Mamlaka wana uelewa wa pamoja wa jinsi wanavyotakiwa kuhudumiwa na nini kinachotarajiwa kutoka kwao.

Misingi hiyo ndiyo imekuwa nguzo kwa Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake na kufikia malengo iliyojiwekea. Msingi namba moja ni Uadilifu ambapo Mamlaka hufuata viwango vya uendeshaji wa hali ya juu katika kila inachofanya kwa kutambua kuwa, uaminifu ni muhimu kwa mafanikio endelevu ya Taasisi.

“Mamlaka huzingatia Ubunifu kama msingi muhimu na utamaduni wa Mamlaka unaothamini uasili wa uvumbuzi na ubunifu katika kukuza vipaji kwa kuzingatia uwazi na ari. Msingi mwingine ni kuthamini Wateja ambapo Mamlaka hujitoa kwa dhati kuwasaidia wateja wa nje kutimiza malengo yao”, amesema Ndomba na kuongeza kuwa,

Ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, Mamlaka huzingatia msingi wa kufanya kazi kwa pamoja huku kukiwa na mawasiliano sahihi kwa watumishi wote, lengo ni kuhakikisha kila mtumishi anapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu Mamlaka muda wote.

“Kama ambavyo inaeleweka, ushirikiano ni muhimu katika kufikia malengo ya taasisi hivyo Mamlaka husimamia msingi huu wa Ushirikiano kwa kuhakikisha kuwa inafanya

kazi kwa uwazi na Taasisi za Umma na wadau wengine sambamba na kubadilishana taarifa, maarifa, uzoefu na kutambua kuwa Taasisi za Umma na wadau wengine ni muhimu kwa maendeleo ya Serikali Mtandao”, amesema Ndomba na kuhitimisha kuwa “Tunapozungumzia kujenga serikali mtandao tunamaanisha maeneo yote Tanzania Bara na Visiwani na ndio maana sisi Mamlaka ya Serikali Mtandao tunashirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar kuhakikisha tunafanikisha kujenga serikali ya kidigitali”,



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba akitoa ufafanuzi wakati wa mahojiano kuhusu miaka 10 ya Mamlaka hiyo